

BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

TAARIFA FUPI YA MASHAIRI (LYRICS) ZA WIMBO UITWAO KIBANGO

Baraza la sanaa la Taifa (BASATA) limepitia na kuhakiki mashairi ya wimbo uitwao “**KIBANGO**” na kuupa daraja **WZ18** sawa na daraja **A** yaani kusikilizwa na watu wenye umri kuanzia miaka **18** na kuendelea na kusikilizwa sehemu maalumu ambako watu chini ya umri huo hawatokuwepo.

MCHANGANUO WA KANUNI YA 25

Kanuni ya 25 Kifungu cha 6 Inaeleza kuwa Ili wimbo uweze kukubalika na kupelekwa kwenye jamii unatakiwa uwe na vitu vifuatavyo

- a) Hauvunji heshima ya mwimbaji, msikilizaji na mtazamaji.
- b) Hauna upotoshaji wa aina yejote.
- c) Hauchochesi ghasia ya aina yoyote au namna yoyote.
- d) Hauna meneno ya uongo, uchochezi au yanayo kashifu watu wengine.
- e) Hauudhurishi lugha chafu na matusi,
- f) Hautukuzi ubaguzi wa rangi, ukabila au dini.
- g) Haukashifu Taifa la Tanzania au mataifa mengine.
- h) Haudhoofishi umoja, ushirikiano na ustawi bora wa jamii.
- i) unazingatia masharti ya sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya haki za ubunifu na mambo mengine yote.
- j) Haishawishi wala kuhamasisha vitendo vya ngono, ushoga, usagaji au matumizi ya dawa za kulevyo

UHAKIKI WA MASHAIRI YA WIMBO HUU UITWAO KIBANGO

Wimbo ni mzuri kuanzia kwenye upangaji wa vina na mizani, utumiaji wa lugha ya picha na tafsida kama maneno "**Hii party ina vijiti**". Ujumbe wa wimbo huu umelenga zaidi watu wanaotumia vilevi mbalimbali na hii imejidhihirisha katika mashairi kama "**Naskia nyeee nyepesi hii pombe Nchanganyie Bapa**", lakini pia ujumbe mwingine unahu mapenzi. hivyo basi wimbo huu umewalenga watu wenyewe umri kuanzia miaka 18, kutokana na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umri sahihi wa mtu kutumia vilevi na kujihusisha na mapenzi ni kuanzia miaka 18 na kuendela.

Kutokana na Kanuni ya Baraza la Sanaa la Taifa wimbo wa **Kibango** unapewa daraja WZ18 sawa na daraja A yaani ujumbe wake ni mahususi kwa watu wenyewe umri kuanzia miaka 18 na kuendelea na utasikilizwa sehemu maalumu tu ambako watoto au watu chini ya umri wa miaka 18 hawatokuwepo

ANGALIZO:

Kwa vyombo vyaa habari kuzingatia muongozo wa maadili kwenye kucheza wimbo huu na kuzingatia mazingira, muda na aina ya vipindi ambavyo hufuatiliwa na kusikilizwa na watu wenyewe umri kuanzia miaka 18 na kuendelea ili ku

Kwa wazazi, walimu, maeneo ya sherehe na burudani na wadau wote wa Sanaa kuzingatia maadili wakati wa uchezaji wa wimbo huu kama ilivyoshauriwa na Baraza.